



*Namba ya Whatsap: 0752965019/ +255 757 411 482*

# MPANGILIO WA NYAKATI ZA BIBLIA(CHRONOLOGY)

Leo, tutaanza kujifunza somo la **Mpangilio wa Nyakati za Biblia yaani Chronology**. Je, neno "chronology" linamaanisha nini? Neno hili linatokana na maneno mawili: **"chronos"** na **"logos"**. "Chronos" linamaanisha *wakati*; jina la kitaalamu la saa ni *chronometer*, yaani kifaa kinachopima wakati. Na "logos" linamaanisha *elimu au somo*. Hivyo basi, **chronology** inamaanisha ***elimu ya wakati.***

Mpangilio wa nyakati za Biblia ni kujifunza kibiblia kuhusu wakati katika historia ya mwanadamu. Tunajua wazi kuwa sasa tupo zaidi ya miaka 2000 tangu kuanza kwa kipindi kiitwacho **B.K.** (Baada ya Kristo). Na katika kipindi cha **K.K.** (Kabla ya Kristo), je, ni miaka mingapi imepita tangu kuumbwa kwa Adamu? Ni miaka mingapi imepita katika historia ya mwanadamu hapa duniani? Wanasayansi hutoa kauli zinazotofautiana; wengine husema maelfu kwa maelfu ya miaka, huku wengine wakisema makumi ya maelfu ya miaka. Lakini je, idadi halisi ni ipi? Je, Biblia inaonesha jambo hili pia? Ndiyo! Wakati tunapofanya "uchunguzi" katika Kitabu cha Bwana kwa kufuata kanuni ya Mungu ya *"hapa kidogo na pale kidogo,"* tunapata jibu Kwa kutumia **hatua 7** na **viungo 50** (aya).Sasa tuanze kujifunza mpangilio wa nyakati za Biblia kwa;

**Hatua ya 1**: Tangu kuumbwa kwa Adamu hadi Gharika.

## HATUA YA 1: TANGU KUUMBWA KWA ADAMU HADI GHARIKA

Hiki ndicho kipindi cha **Dunia ya Kwanza** katika Mpango wa Mungu. Kipindi halisi cha muda wa kipindi hiki kimeelezwa kwetu na Mungu katika sura ya ajabu ya Mwanzo, **Sura ya 5**. Wengi wamewahi kushangazwa na maelezo ya sura hii kuhusu ukoo, na baadhi hata wamewahi kudhani kwamba sura hii haina maana yoyote! Lakini kama sura hii haingekuwepo katika Biblia, basi tusingewahi kujua muda wa kipindi cha Dunia ya Kwanza ulikuwa wa muda gani! Ndiyo, tusingewahi kujua kipindi kilichopita tangu kuumbwa kwa Adamu hadi Gharika kilikuwa kirefu kiasi gani.

Sasa, je, tunaanzaje kufanya hesabu hizi? Je, tunajumlisha umri wa watu 10 waliotajwa katika mlolongo wa Adamu kuanzia Sethi? Tukifanya hivyo, tutapata idadi kubwa sana, na zaidi ya hapo, tungekuwa tunarudia na kurundika vipindi vilevile vya muda ambavyo vilishafunikwa wakati walipoishi pamoja katika kipindi kilekile cha muda. Kwa mfano, wakati Adamu alipokuwa na umri wa miaka 325, mjukuu wake mkubwa Kenani alizaliwa. Lakini katika miaka hiyo 325, alikuwa akiishi pamoja na mwanawe Sethi kwa miaka 195, na na mjukuu wake Enoshi kwa miaka 90. Hivyo basi, maisha ya watu hawa watatu yalichanganyana katika vipindi fulani vya muda. Kwa hiyo, kwa kipindi halisi cha miaka 325, kama tukijumlisha umri wa watu hao watatu, tungepata: 325 (Adamu) + 195 (Sethi) + 90 (Enoshi) = 610! Lakini muda halisi uliopita ulikuwa ni miaka 325 tu.

Hali hii pia ingekuwa hivyo hivyo ikiwa tungejumlisha umri wa watu wote 10 wa vizazi kumi kutoka Adamu hadi Nuhu.

Basi tufanyeje? Tunapaswa kujumlisha tu idadi ya miaka (au umri) wa kila mtu hadi kuzaliwa kwa mzaliwa wake wa kwanza. Hivyo, tutakuwa na mnyororo wa viungo vya vizazi tisa hadi kuzaliwa kwa Nuhu. Kisha tunapaswa kuongeza kwa idadi hiyo umri wa Nuhu ilipofika wakati wa Gharika, na tutapata idadi ya miaka kutoka kuumbwa kwa Adamu hadi siku Gharika ilipoanza! Ndiyo, ni rahisi kiasi hicho! Adamu aliishi hadi au alikufa wakati Lameki alipokuwa na umri wa miaka 56.

Basi, hesabu ni kama ifuatavyo:

**Adamu** (*Mwanzo 5:3*) alikuwa na umri wa miaka **130** alipo mzaa **Sethi**.

**Sethi** (*Mwanzo 5:6*) alikuwa na umri wa miaka **105** alipo mzaa **Enoshi**.

**Enoshi** (*Mwanzo 5:9*) alikuwa na umri wa miaka **90** alipo mzaa **Kenani**.

**Kenani** (*Mwanzo 5:12*) alikuwa na umri wa miaka **70** alipo mzaa **Mahalaleli**.

**Mahalaleli** (*Mwanzo 5:15*) alikuwa na umri wa miaka **65** alipo mzaa **Yaredi**.

**Yaredi** (*Mwanzo 5:18*) alikuwa na umri wa miaka **162** alipo mzaa **Enoki**.

**Enoki** (*Mwanzo 5:21*) alikuwa na umri wa miaka **65** alipo mzaa **Methusela**.

**Methusela** (*Mwanzo 5:25*) alikuwa na umri wa miaka **187** alipo mzaa **Lameki**.

**Lameki** (*Mwanzo 5:28*) alikuwa na umri wa miaka **182** alipo mzaa **Nuhu**.

**Nuhu** (*Mwanzo 7:11*) alikuwa na umri wa miaka **600** wakati wa Gharika.

**Jumla** ya miaka ni:
130 + 105 + 90 + 70 + 65 + 162 + 65 + 187 + 182 + 600 = **1656**

Kwa hiyo, kipindi cha **Dunia ya Kwanza** kilikuwa na muda wa miaka **1656**.

## HATUA YA 2: KUTOKA GHARIKA HADI KUTOLEWA KWA AHADI

Hiki ni kipindi kinachoanza siku ya kuanza kwa Gharika na kuendelea hadi **"ahadi"**. Je, "ahadi" inayozungumziwa hapa ni ipi? Je, ni ile ahadi iitwayo **"Ahadi ya Ibrahimu"** ambayo Mungu alimpa Ibrahimu mlimani Moria alipokuwa karibu kumtoa sadaka Isaka? Jibu ni **hapana**. Ahadi inayozungumziwa hapa ni **ahadi ya awali** ambayo Mungu alimpa **Abramu** alipokuwa bado katika nchi ya **Uri wa Wakaldayo**. Tunasoma kuhusu hilo katika *Mwanzo 12:1-3*:

*"Nami nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa, nitakubariki, na kulikuza jina lako; nawe utakuwa baraka. Nami nitawabariki wakubarikio, na kumlaani akulaaniye; na katika wewe jamaa zote za dunia watabarikiwa."*

Ndiyo! Hii ndiyo ahadi hiyo. Hii ilikuwa ni ahadi aliyopatiwa Abramu, akiamriwa aondoke katika "nchi yake... na jamaa zake... na nyumba ya baba yake" ili apokee baraka kuu kama angelitii. Hivyo basi, Abramu alipoondoka katika nchi hiyo "kama Bwana alivyomwambia," huo ndio ulikuwa **muda wa kutolewa kwa ahadi**.

Maelezo ya jambo hili tunayasoma katika *Mwanzo 12:4*:

*"Basi Abramu akaondoka, kama Bwana alivyomwambia... Naye Abramu alikuwa na umri wa miaka sabini na mitano alipoondoka Harani."*

Alikuwa na umri wa **miaka 75** wakati huo. Pia, jambo hili lilitokea **mara baada ya baba yake Tera kufa**, kama tunavyosoma sehemu nyingine katika *Matendo 7:4*:

*"Ndipo alipotoka katika nchi ya Wakaldayo, akakaa Harani. Na kutoka huko, baada ya kifo cha baba yake, alihamishwa mpaka nchi hii mnayokaa sasa."*

Hivyo basi, **kipindi hiki cha hatua ya pili kinahesabiwa hadi kufa kwa Tera**, ambapo ndipo **Abrahamu aliposhikilia ahadi** kwa kuondoka katika nchi yake na watu wake.

Hivyo basi, hesabu za hatua hii ya Mpangilio wa Nyakati za Biblia zinapatikana katika **sura ya 11 ya Mwanzo** kama ifuatavyo:

Miaka **miwili baada ya Gharika kuanza** (*Mwanzo 11:10*), **Arfaksadi** alizaliwa (mwana wa Shemu).

**Arfaksadi** (*Mwanzo 11:12*) alikuwa na umri wa **miaka 35** alipozaa **Shela**.

**Shela** (*Mwanzo 11:14*) alikuwa na umri wa **miaka 30** alipozaa **Eberi**.

**Eberi** (*Mwanzo 11:16*) alikuwa na umri wa **miaka 34** alipozaa **Pelegi**.

**Pelegi** (*Mwanzo 11:18*) alikuwa na umri wa **miaka 30** alipozaa **Reu**.

**Reu** (*Mwanzo 11:20*) alikuwa na umri wa **miaka 32** alipozaa **Serugi**.

**Serugi** (*Mwanzo 11:22*) alikuwa na umri wa **miaka 30** alipozaa **Nahori**.

**Nahori** (*Mwanzo 11:24*) alikuwa na umri wa **miaka 29** alipozaa **Tera**.

**Tera** (*Mwanzo 11:32*) alikufa akiwa na umri wa **miaka 205**.

**Jumla** ya miaka ni:
2 + 35 + 30 + 34 + 30 + 32 + 30 + 29 + 205 = **427**

Kwa hiyo, kipindi kutoka **Gharika hadi Ahadi** ni **miaka 427**.

## HATUA YA 3: TANGU AHADI HADI KUTOLEWA KWA SHERIA

Kipindi hiki au hatua hii inaanzia pale ambapo hatua iliyopita ilishia—**Abramu alipoondoka katika nchi ya baba yake baada ya kifo cha baba yake**, na kinaendelea hadi **kutolewa kwa sheria**. Kumbuka hakuna pengo katika mnyororo wa viungo vya hatua hizi! Sasa, je, sheria ilitolewa lini? Wengi watadhani ni pale mlimani Sinai ambapo Musa alipokea Amri Kumi. Lakini sivyo ilivyo. Hii inahusu kutolewa kwa **sheria ya kwanza**, ambayo ilikuwa **usiku wa mwisho kabla ya Waisraeli kutoka Ramesesi huko Misri**.

Tunaona na kusoma juu ya jambo hili katika *Kutoka 12:41-43*:

*"Ikawa mwisho wa miaka mia nne na thelathini, hata siku iyo hiyo, majeshi yote ya Bwana yalitoka katika nchi ya Misri. Ni usiku wa kushikamana kwa ajili ya Bwana, kwa kuwa aliwatoa katika nchi ya Misri; ndio usiku wa Bwana wa kushikamana kwa wana wa Israeli, vizazi vyao vyote. Bwana akawaambia Musa na Haruni, Hii ndiyo sheria ya pasaka; hakuna mgeni atakayekula hiyo."*

Je, umeona hilo? Ilikuwa ni **"sheria ya Pasaka"**, yaani **sheria ya kwanza ya Mungu kwa Israeli**! Ndiyo! Hii ndiyo sheria ya kwanza aliyowapa Mungu Israeli—**Sheria kutoka kwa Mungu**!

Sasa, kipindi hiki cha muda kilikuwa cha miaka mingapi? Tunaona jibu lake katika Agano Jipya, kwenye *Wagalatia 3:17*:

*"Basi nasema hivi, ya kuwa agano lililofanywa zamani na Mungu, halibatilishwi na sheria iliyokuja baada ya miaka mia nne na thelathini, hata kuibatilisha ile ahadi."*

Hii inazungumza waziwazi kuwa kipindi kati ya **Ahadi na Sheria** ni **miaka 430**. Lakini pia kuna njia nyingine ya kupata idadi hii. Tunasoma kuhusu hilo katika *Kutoka 12:40*:

*"Basi muda wa wana wa Israeli waliokaa Misri ulikuwa miaka mia nne na thelathini."*

Inawezekanaje hivyo? Yakobo alipoingia Misri walikuwa jumla ya watu sabini wote (*Mwanzo 46:2*), na kwa vizazi vitatu tu (Lawi – Kohathi – Amramu – Musa, *1 Nyakati 6:1-3*), inawezekanaje kipindi hicho kiwe miaka 430? Ili kuelewa aya hii, tunapaswa kutambua kwa makini kuwa miaka 430 haikuwa kipindi cha kukaa Misri tu, bali **ilijumuisha na kipindi cha kabla yake pia**.

*"Na muda wa wana wa Israeli, waliokaa Misri, ulikuwa miaka mia nne na thelathini"*
*(tafsiri halisi ya Strong's – Agano la Kale).*

Ibrahimu, Isaka, Yakobo na wana wao, ingawa walikuwa ndani ya nchi ya Kanaani, waliishi na kuhamahama kama wageni kutoka sehemu moja hadi nyingine. Hivyo basi, **miaka 430 ilianza tangu mwaka ambapo Ibrahimu aliingia Kanaani**.

Zaidi ya hapo, kama vile Lawi alivyotoa zaka akiwa bado katika viuno vya Ibrahimu, ndivyo pia wana wa Israeli walivyotembea kama wageni wakisubiri ahadi kutimia wakiwa ndani ya Ibrahimu, Isaka na Yakobo kwa miaka 430 (*Waebrania 7:9-10*). Ingawa walikuwa bado hawajazaliwa, Israeli kama taifa walikuwa **wameahidiwa ardhi yao**

**wenyewe** wakiwa ndani ya viuno vya Ibrahimu, na hivyo wakaishi kama **wapitaji** wakisubiri kutimizwa kwa ahadi.

Ibrahimu alikuwa na umri wa miaka **75** (*Mwanzo 12:1, 2, 4, 5, 7*) alipoingia Kanaani. Walikaa Kanaani kwa miaka **215**, kisha wakakaa Misri kwa miaka **215**, na kufanya jumla ya **miaka 430** (*Wagalatia 3:17, Kutoka 12:41*). Miaka hii 430 inakamilika na **kutolewa kwa sheria ya Pasaka**.

Hivyo basi, kutoka **Ahadi hadi Kutolewa kwa Sheria** ni kipindi cha **miaka 430**.

## HATUA YA 4: TANGU KUTOLEWA KWA SHERIA HADI MGAWANYO WA ARIDHI

Hiki ni kipindi cha muda kinachoanza mahali pale pale ambapo hatua iliyopita ilimalizika! Ni usahihi wa ajabu wa Mungu! Hatua hii inahusu kipindi kinachoanzia usiku wa mwisho nchini Misri, ambapo sheria ya Pasaka ilishikwa, hadi kukamilika kwa mgawanyo wa aridhi ya Kanaani kwa makabila 11. (Kabila la Lawi halikupewa sehemu katika nchi—ndiyo maana walipokea sehemu ya kumi ya mali kutoka kwa wengine—*Hesabu 18:26*).

Kuna hatua tatu za msingi kwa ajili ya kufanya hesabu hii:

1. Safari kutoka Ramesesi huko Misri (*Hesabu 33:3*) hadi Mlima Sinai ilichukua mwaka mmoja. Maandiko katika *Hesabu 33:3* na *Hesabu 10:11-13* yanaonesha wazi muda huu.

2. Kutangatanga jangwani kulidumu kwa miaka 39 ya ziada. *Hesabu 14:33* inarejelea kipindi cha adhabu cha miaka 40; kwa kuwa walikuwa tayari jangwani kwa mwaka mmoja, kipindi hiki kilikuwa miaka 39.

3. Mgawanyo wa aridhi ulidumu kwa miaka 6. Katika *Yoshua 14:7* na *Yoshua 14:10*, Kalebu anazungumza kuhusu miaka 45 iliyopita tangu yeye na wengine kumi na mmoja walitumwa kupeleleza nchi ya Kanaani (*Hesabu 13:6*) hadi wakati wa kugawa aridhi. Miaka hii 45 ilianza wakati Israeli walikuwa Mlima Sinai. Hivyo basi, kipindi cha "mgawanyo wa aridhi" kinahesabiwa kama miaka 45 (jumla ya muda tangu kupeleleza) pungufu ya miaka 39 (miaka ya kutangatanga jangwani baada ya mwaka wa kwanza Sinai), ambayo ni sawa na miaka 6.

Kwa hiyo, jumla ya kipindi hiki ni mwaka 1 + miaka 39 + miaka 6 = miaka 46.

Kipindi tangu Kutolewa kwa Sheria hadi Mgawanyo wa Nchi ni miaka 46.

## HATUA YA 5: KIPINDI CHA WAAMUZI

Hiki ni kipindi kati ya kukamilika kwa mgawanyo wa aridhi na kuendelea hadi kutiwa mafuta kwa mfalme wa kwanza wa Israeli—Sauli. Katika kipindi hiki cha muda, Mungu aliwapa Israeli waamuzi. Waamuzi hawa walikuwa viongozi wa kuwaongoza Israeli.

Mwamuzi wa kwanza alikuwa Yoshua (*Hesabu 27:22-23*). Mwamuzi wa mwisho alikuwa nabii Samweli.

Kipindi cha hawa waamuzi kilikuwa cha muda gani? Taarifa hii haipatikani katika Agano la Kale bali imetolewa na Mungu Mwenyewe kupitia Roho Mtakatifu katika Agano Jipya kwa kinywa cha Mtume Paulo katika *Matendo 13:20*:

*"Baada ya hayo akawapa waamuzi kwa muda wa miaka mia nne na hamsini, hata wakati wa nabii Samweli."*

Tafadhali tambua maneno haya—"baada ya hayo." Hii inaashiria nini? Inatuthibitishia kuwa hesabu ya kipindi hiki inaanza tu **baada ya mgawanyo wa aridhi**, kama inavyothibitishwa katika aya iliyotangulia, *Matendo 13:19*:

*"Na alipokuwa amewaangamiza mataifa saba katika nchi ya Kanaani, aliwagawia nchi yao kwa kura."*

Hii ipo wazi kabisa! Kipindi cha waamuzi kinaoneshwa kuwa ni miaka 450.

Maneno "kwa muda wa" yanaonekana kuonesha kuwa ni makadirio ya takriban na si muda kamili halisi wa kipindi cha waamuzi. Kwa nini iwe hivyo? Uchunguzi wa karibu wa jambo hili utaonesha kuwa kipindi hiki cha miaka 450 kilichotolewa na Mungu si muda halisi wa urefu wote wa enzi ya waamuzi. Kwa nini?--Kwa sababu mwanzoni na mwishoni mwa kipindi hiki cha waamuzi, kuna maeneo yanayochanganyika na hatua zilizo kabla na baada katika mpangilio wa nyakati wa Biblia.

Yoshua, Mwamuzi wa kwanza, alitiwa mafuta na Musa kuwa Mwamuzi kabla ya kuingia Kanaani, na alikuwa mwamuzi wakati wa mgawanyo wa aridhi (miaka sita) na hata baada ya wakati ambapo

Kalebu alitamka maneno hayo (*Yoshua 14:10*). Aidha, Samweli, mwamuzi wa mwisho, aliendelea kuwa mwamuzi hadi alipokufa, baada ya Sauli kuanza kutawala kama Mfalme wa Israeli (utawala wa Sauli ulikuwa wa miaka 40).

Kipindi cha miaka 450 cha *Matendo 13:20*, "kwa muda wa," kinarejelea muda kutoka **baada ya mgawanyo wa aridhi** hadi **Sauli alipotiwa mafuta kuwa mfalme**, na si kipindi chote cha maisha ya waamuzi wote. Hivyo basi, ndivyo Mungu anavyotoa muda "baada ya hayo" (*Matendo 13:20*)—yaani baada ya mgawanyo wa aridhi—hadi sehemu ya kazi ya Samweli kabla ya utawala wa Sauli kuanza, au hadi siku ya kutiwa mafuta kwa Sauli kuwa mfalme. Hiki ndicho kipindi cha muda kinachohitajika kwa ajili ya hatua ya tano ya hesabu ya mpangilio wa nyakati wa Biblia.

Lakini kama tulivyoona sasa, hiki si kipindi halisi kamili cha enzi ya waamuzi wote, ambayo ni ndefu zaidi na ina vipindi vya mchanganyiko mwanzoni na mwishoni. Hivyo basi, Mungu kwa usahihi na hekima kubwa kabisa anatumia maneno "kwa muda wa" (akiashiria marekebisho aliyoyafanya), kwa kuwa aliondoa vipindi vya mchanganyiko na kutupa kipindi halisi cha hesabu tunachokihitaji.

Kipindi cha Waamuzi, kama kinavyohitajika katika mpangilio wa nyakati za Biblia, ni miaka 450.

# HATUA YA 6: KIPINDI CHA WAFALME

Hiki ni kipindi cha wafalme kinachoanza na mfalme wa kwanza, Sauli, hadi anguko la mfalme wa mwisho wa Yuda, Sedekia.

Mpangilio wa wafalme watatu wa kwanza na muda wa kutawala kwao ni kama ifuatavyo:

Sauli (*Matendo 13:21*) alitawala kwa miaka 40.
Daudi (*1 Mambo ya Nyakati 29:27*) alitawala kwa miaka 40.
Solomoni (*1 Wafalme 11:42* au *2 Mambo ya Nyakati 9:30*) alitawala kwa miaka 40.

Baada ya kifo cha Mfalme Solomoni, Israeli iligawanyika kuwa mataifa mawili: Israeli (makabila 10) na Yuda (makabila 2). Kwa kipindi kilichobaki cha mpangilio huu wa nyakati, tutaendelea kufuatilia mlolongo wa wafalme wa Yuda, ambao juu yao neema ya Mungu ilikuwapo, kwa kuwa kutoka kwa Yuda angekuja Masihi, "Shilo" (*Mwanzo 49:10*).

Hapa chini ni orodha ya wafalme wa Yuda kuanzia na mwana wa Solomoni, Rehoboamu, na muda wao wa kutawala:

Rehoboamu (*2 Mambo ya Nyakati 12:13*) – miaka 17
Abiya (*2 Mambo ya Nyakati 13:2*) – miaka 3
Asa (*2 Mambo ya Nyakati 16:13*) – miaka 41
Yehoshafati (*1 Wafalme 22:42*) – miaka 25
Yehoramu (*2 Wafalme 8:17*) – miaka 8
Ahazia (*2 Wafalme 8:26*) – mwaka 1
Athalia (*2 Wafalme 11:3*) – miaka 6
Yoashi (*2 Wafalme 12:1*) – miaka 40
Amasia (*2 Wafalme 14:2*) – miaka 29
Azaria (Uzia) (*2 Wafalme 15:2*) – miaka 52
Yothamu (*2 Wafalme 15:33*) – miaka 16
Ahazi (*2 Wafalme 16:2*) – miaka 16
Hezekia (*2 Wafalme 18:2*) – miaka 29
Manase (*2 Wafalme 21:1*) – miaka 55
Amoni (*2 Wafalme 21:19*) – miaka 2
Yosia (*2 Wafalme 22:1*) – miaka 31
Yehoahazi (*2 Wafalme 23:31*) – robo mwaka (miezi 3)
Yehoiakimu (*2 Wafalme 23:36*) – miaka 11
Yehoiakini (*2 Wafalme 24:8*) – robo mwaka (miezi 3)
Sedekia (*2 Wafalme 24:18*) – miaka 11

Kwa hiyo, kipindi hiki cha wafalme kinajumlisha miaka 513. (Tafadhali kumbuka: miezi 6 ya ziada au sehemu ya mwaka kutoka kwa Yehoahazi na Yehoiakini hazijahesabiwa mara mbili katika jumla hii bali ni sehemu ya kipindi cha utawala wao; hesabu ya jumla inafikiwa kwa kujumlisha miaka kamili tu, sehemu ndogo za miaka zimezingatiwa ndani ya mzunguko mzima wa mfululizo bila kusababisha jumla kama vile 513.5).

Kipindi cha Wafalme ni miaka 513.

## HATUA YA 7: TANGU MWISHO WA KIPINDI CHA WAFALME HADI MWAKA 1 B.K.

Kipindi hiki cha mwisho kinaanza na anguko la mfalme wa mwisho wa Yuda, Mfalme Sedekia (karibu mwaka 606 K.K., ingawa kuanguka kwa mwisho kwa Yerusalemu kulikuwa mwaka 586 K.K.), na kinatupeleka moja kwa moja hadi mwaka 1 B.K.

Sasa hebu tuangalie hatua hii ya mwisho ya Mpangilio wa Nyakati za Biblia. Baada ya anguko la Mfalme Sedekia, kama tunavyosoma katika *2 Mambo ya Nyakati 36:20-21*:

*“Nao waliookoka kwa upanga akawachukua mpaka Babeli... ili kutimiza neno la Bwana... kwa muda wa miaka sabini.”*

Ndiyo! Mateka wa Waisraeli huko Babeli walikaa kipindi cha miaka 70. Kisha, katika mwaka wa kwanza wa utawala wa mfalme wa Uajemi, Mfalme Koreshi, watu waliachiliwa huru. Tazama 2 *Mambo ya Nyakati 36:22-23*:

*"Basi katika mwaka wa kwanza wa Koreshi, mfalme wa Uajemi... Bwana aliichochea roho ya Koreshi, mfalme wa Uajemi, naye akatangaza agizo... akisema... Ni nani katika ninyi aliye wa watu wake wote? Bwana, Mungu wake, na awe pamoja naye, naye na apande juu."*

Tarehe hii ya mwaka wa kwanza wa Mfalme Koreshi inajulikana vizuri na imerekodiwa katika historia ya kidunia kuwa ni mwaka **536 K.K.** Ndiyo! Mungu anatuchukua kwa mkono na kutuongoza kupitia Neno lake hadi tufike kwenye eneo la hakika na la kutegemewa la mpangilio wa nyakati wa historia ya kawaida. Hii ni sawa kabisa na namna mtu anavyomwelekeza na kumsindikiza mtu mwingine anayeulizia njia ya kwenda mahali hadi atakapofika mahali anapopajua, na hapo anaweza kuendelea mwenyewe. Ndiyo! Mungu naye ametufanyia vivyo hivyo leo!

Kwa hiyo, kipindi cha muda wa hatua hii ya mwisho ya Mpangilio wa Nyakati za Biblia kuanzia mwanzo wa mateka wa miaka 70 (ambayo mara nyingi huhesabiwa kuanzia mwaka 606 K.K. kwa kupelekwa kwa kundi la kwanza) hadi tamko la Koreshi (536 K.K.), halafu kutoka kwa tamko la Koreshi hadi mwaka 1 B.K., huhesabiwa kama:

**Miaka 70** (mateka) + **Miaka 536** (kutoka 536 K.K. hadi 1 B.K.) = **Miaka 606**.

**Jumla ya Miaka Toka Kuumbwa kwa Adamu hadi Tarehe 1 Januari, Mwaka 1 B.K.**

1656 (Hatua ya 1) + 427 (Hatua ya 2) + 430 (Hatua ya 3) + 46 (Hatua ya 4) + 450 (Hatua ya 5) + 513 (Hatua ya 6) + 606 (Hatua ya 7) = **Miaka 4128**.

Kwa hiyo, tunajua kwamba **Adamu aliumbwa mwaka 4128 K.K.**

Hivyo basi, kutoka katika "Kitabu cha Bwana"—yaani Biblia—tumepata kwa mnyororo usiovunjika wa viungo na aya 50, kipindi cha muda kilichopita tangu kuumbwa kwa Adamu hadi mwaka 1 B.K.


Ndiyo! Mungu Mwenyewe ametufunulia mpangilio sahihi wa nyakati kutoka katika Neno lake, kama alivyotuahidia katika *Isaya 34:16*:

*"...hapana hata moja ya hayo itakayokosa mwenzi wake; kwa kuwa kinywa changu kimeamuru, na roho yake imewakusanya."*

Ndiyo! Neno limetufunulia leo hesabu ya "saa kuu ya wakati" ya Mungu kwa mwanadamu. Na sisi tunaamini, kwa kuwa:

*"...neno lako ni kweli."* (*Yohana 17:17*)

Amina



*Kwa Masomo zaidi Tuandikie Ujumbe kupitia:*

*Email: thekingdom1_6@gmail.com au isayaruhala25@gmail.com*

*©HAKIUZWI*

***Namba ya Whatsap: 0752965019/ +255 757 411 482***